**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA.

**JUNI, 2024**

**DODOMA.**

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA,**

**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU,**

**S.L.P 67,**

**KATESH.**

**TAREHE………………………**

**NAMBA ZA SIMU.**

- **MKUU WA SHULE 0784-844092**
- **M/MKUU WA SHULE 0755-900058.**
- **MWANDAMIZI TAALUMA 0754-775502**
- **MWANDAMIZI MALEZI 0762-811220**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

**………………………………….**

**S.L.P……………**

**YAH:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU MWAKA 2024.**

1. **Utangulizi.**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao……………………………………amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Balang'dalalu mwaka 2024 tahasusi ya HGL/HGLi.

Shule ipo halmashauri ya wilaya ya Hanang', mkoa wa Manyara kilometa 22 kusini mwa barabara kuu ya Arusha-Singida.

Hivyo unapokuja utashukia stendi ya mabasi ya katesh na kupanda magari ya abiria yanayokuja Balang'dalalu sekondari kwa nauli ya shilingi 3000 tu kwa magari ya abiria.

Wanafunzi wote wa kidato 2024 wanatakiwa kuripoti shuleni kuanzia Julai 01, 2024 kwa ajili ya kupewa maelekezo muhimu ya kozi yao (orientation course). **MUHULA WA MASOMO UNAANZA TAREHE 01, Julai 2024**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14 Julai 2024.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**.

**Sare;-**

Shule ya sekondari Balang'dalalu inatumia sare za aina mbili, ambazo ni sare ya darasani na sare ya kazi ya nje (shamba dress). Sare ya darasani inapatikana shuleni kwa bei rafiki. Sare ya kazi za nje (shamba dress) mzazi/mlezi atamnunulia mwanae huko atokapo kabla ya kuripoti hapa shuleni. Shule imebeba jukumu hilo ili kulinda nidhamu ya uvaaji sare kwa wanafunzi wetu,

muonekano na haiba ya wanafunzi wetu wanapokuwa shuleni na nje ya shule. Ni mwiko kuja shuleni na mavazi ya nyumbani.

** tafadhali kumbuka sare ya darasani inapatikana shuleni usisumbuke**.

Sare ya **kazi za nje (shamba dress)-nunua sare hii ukiwa nyumbani na uje shuleni ukiwa umeivaa, usije shuleni ukiwa umevaa mavazi ya nyumbani kwa sababu HUTOPOKELEWA, SARE YA KAZI ZA NJE (shamba dress).**

- Suruali mbili za kitambaa cha khaki zenye marinda mawili kulia na kushoto, mfuko mmoja nyuma.
- T-shirt mbili za bluu (royal blue) zenye kola isiyo na maandishi yeyote.

**SARE YA DARASANI (classroom uniform).**

- Wavulana: suruali mbili rangi ya kijani jeshi zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji.
- Mashati 02 rangi nyeupe cotton ya mikono mirefu.
- Masweta mawili rangi ya bluu (blue) yenye mikono mifupi yenye nembo ya shule, yanapatikana shuleni kwa atakayehitaji.
- Tshirt 02 rangi nyekundu, zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji, (hii ni sare ya darasani inavaliwa jumatano na ijumaa).
- Tai mbili ndefu rangi bluu yenye mistari myeupe (special tai) zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji.
- Track suit moja rangi bluu (royal blue) inapatikana shuleni kwa atakayehitaji (track suit)
- Viatu vyeusi jozi mbili vya kufunga gidamu vyenye visigino vifupi, isiwe buti, nunua uje navyo. Soksi za rangi ya khaki au nyeusi jozi mbili. Nunua uje nazo.

**ZINGATIA:**

- **Mavazi yote yaliyoorodheshwa hapo juu ndiyo yatakayoruhusiwa shuleni na si vinginevyo.**
- **VITAMBAA vyote vya kushonea sare ya darasani, masweta, mashati, track suit na Tshirt zinapatikana shuleni kwa atakayehitaji.**
- **Suruali zishonwe ndefu zinazofunika viatu upana chini usioungue nchi 14 iwe na rinda mbili kulia na kushoto nyuma iwe na mfuko mmoja.**

****SARE ZA SHULE NI JOZI MOJA MOJA (mbili mbili) ISIPOKUWA TRACK SUIT TU**

****VITAMBAA NA SWETA, TSHIRT TRACK SUIT ZINAPATIKANA SHULENI KWA BEI RAFIKI KWA MZAZI ATAKAYEHITAJI HUDUMA HIYO.**

**VIFAA VYA MALAZI.**

Kila mwanafunzi anunue aje navyo;-

- Godoro 01 lenye upana wa futi mbili na nusu na unene wa “4” (nchi 4) nunua godoro lenye ubora.

- Mashuka mawili ya rangi bluu.
- Blanketi moja.
- Mto mmoja wenye foronya unaofanana na shuka.
- Chandarua kimoja ili kujikinga na mbu.

**VIFAA VYA TAALUMA.**

- Kila mwanafunzi aje na madaftari counter books 10 (kumi).
- Madaftari madogo ya mazoezi 08 (nane).
- Kamusi ya lugha ya kiingereza (advanced learners dictionary)
- Vitabu vya masomo ya tahasusi yako i.e History, Geography, English and general studies.
- Kalamu 10, penseli 10, rula ndefu 2.
- Begi moja la kubebea vifaa vya darasani.
- Kila mwanafunzi alete rim pepa mbili, moja ya photocopy (size A4) na moja ya mistari (A4 rulled paper).

**VIFAA VINGINE.**

- Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe, kijiko vyote viwe vya bati.
- Sanduku moja kubwa (tanka) la bati au chuma, nunua sanduku imara la kufunga na kufuli mbili ( vitasa viwili).
- Uje na ndoo mbili moja kubwa na moja ndogo.
- Uje na jembe moja lenye mpini
- Nunua panga moja jipya uje nalo
- Ufagio, dekio (mop) moja.
- Uje na BIMA ya afya kwa ajili yako au Tsh.50400/= kwa ajili ya bima ya afya uwapo hapa shuleni.

| **Na** | **Aina ya mchango** | **kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65000/= |
| **2** | tahadhari | 5000/= |
| **3** | nembo | 5000/= |
| **4** | Kitambulisho cha shule | 5000/= |
| | **Jumla** | **80000/=** |

**FEDHA hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule NMB**

**NAMBA 41001200091.**

- **JINA LA AKAUNTI NI SHULE YA SEKONDARI BALANG’DALALU.**
- Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye slip ya benki wajati unalipa.

**Sheria na kanuni za shule.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;-

**Sheria na kanuni za shule.**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nan je ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni;

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa.kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa).

**Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua au kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na fomu muhimu.**

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali;
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
**iv.** Picha nne (04) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu;

**Tafadhali soma kwa makini:**

**MAAGIZO.**

- Kila mwanafunzi lazima asome sheria, kanuni na taratibu za shule kwa uangalifu azifuate na kutii. kutofanya hivo ni makosa.
- Uvunjaji wa sheria yoyote ya shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa.
- Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote na afanye mazoezi na mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake. Ni kosa linaloweza kumfukuza mwanafunzi shuleni kwa kuacha kuhudhuria vipindi na kuacha kufanya mazoezi/mitihani bila sababu za msingi.

**Sheria za bweni.**

a) Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/kupika bwenini aidha kwa kutumia moto wa kuni, mkaa, mafuta ya taa au moto wa umeme.
b) Bwenini ni mahali pa kulala si pa kupiga kelele. Mazungumzo ya bwenini yawe mazungumzo ya maana na yawe na sauti ndogo. Upigaji kelele au mayowe ni viashiria vya uhuni, fujo n.k hiyo haikubaliki.
c) Usafi wa bweni ndani na nje (mazingira yanayozunguka bweni ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika).

d) Ni makosa kukaribisha mgeni yeyote bwenini au katika eneo la bweni.
e) Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi.
f) Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wana-bweni wote kulinda sharia kwa kuzitekeleza kwa vitendo.
g) Mwanafunzi haruhisiwi kumiliki bwenini vyombo vifuatavyo **redio, pasi, heater, camera, simu ya mkononi, hotpot,walk man au kifaa chochote cha muziki, sufuria, pombe, madawa ya kulevya, manukato (perfume).**

**NB: mwanafunzi atakayekutwa na vitu tajwa hapo juu atachukuliwa hatua kali. Unaweza kuja na chupa ndogo ya chai (thermos).**

**N.B:** kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu ambao hujitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa, **TAFADHALI UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KUHUSIKA KWA NAMBA ZA SIMU ULIZOPEWA KWENYE FOMU HII.**

**VIAMBATANISHO MUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI.**

- Fomu ya mapokezi na utambulisho (joining instruction form).
- Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form); IJAZWE NA HOSPITALI YA SERIKALI.
- Cheti cha matokeo ya kidato cha nne (result slip).
- Picha passport size 03.
- Risiti ya benki kuonesha malipo ya mchango.

**Tafadhali soma kwa makini sheria za shule zilizoambatanishwa na fomu hii.**

**KARIBU SANA SHULE YA BALANG’DALALU, SHULE YA SEKONDARI.**

……………………………………………..

**MWL.YUDA A. FISSOO**

**MKUU WA SHULE.**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

**BALANG'DALALU SECONDARY SCHOOL**

**P.O BOX 67**

**KATESH.**

**HANANG-MANYARA**

**DATE:………………….**

**REF: NO, BSS/MED/VOLI/2024**

**<u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.</u>**

**TO THE MEDICAL OFFICER……………………………….........................................**

**…………………………………………………………………………………………….**

Please examine………………………………………. (name of student) who has been selected to join this school for his fitness as a student in the following: -

(To be completed by a medical officer)

1. Eye sight……………………………………………
2. Hearing ………………………………………………
3. Limbs ………………………………………………
4. SPECIMENi) stool………… ii) urine………… iii) blood………………..
   iv) Neurosis…………..
5. Asthma…………………………
6. Tuberculosis……………………
7. Pregnancy……………………..
8. Other serious diseases i) venereal disease………………ii) leprosy…………
   iii) Epilepsy……………….iv) Ulcers…………………

MEDICAL CERTIFICATE.

(To be completed by a medical officer) I have examined the above and consider him/her to be physically fit/unfit as a student.

Date……………………….. Signature……………………

Station………………….. Designation…………………….

NB: I request this form to be returned to the school in a sealed-envelope

…………………………….

THE HEADMASTER.

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI**

**MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI (IRUDISHWE SHULENI)**

**SEHEMU: “A”-Ijazwe na mwanafunzi;**

**Jina la mwanafunzi (majina matatu)…………………………………………**

**Anuani………………………………….**

**Taifa/uraia…………………………………………………**

**Dini……………………………………………….**

**Tarehe ya kuzaliwa……………………………jinsia………………………….**

**Shule anakotoka (shule ya sekondari)………………………kata ya……………………..**

**Mwaka wa kumaliza kidato cha nne………………………..**

**Wilaya anakotoka………………………………..**

**Mkoa……………………………….**

**SEHEMU: “B” ijazwe na mzazi/mlezi**

**Jina la mzazi/mlezi (majina matatu)………………………………………………….**

**Anuani ya mzazi/ mlezi……………………………….**

**Namba ya simu ya mzazi/mlezi……………………………………**

**Mahali anapoishi……………………………………………..**

**Kazi ya mzazi/mlezi………………………………….**

**Mahali anapofanya kazi…………………………………….**

**Ndugu wawili wa karibu(wanaoweza kushika nafasi ya mzazi/mlezi)……………………**

**…………………na……………………………………………..**

**SEHEMU “C”**

- **Tafadhali fika na vifaa vyote ulivyoagizwa**
- **wahi shuleni kabla ya saa 11:00 jioni.**
- **Mzazi hakikisha unakamilisha malipo yote kabla ya kuleta mwanao shuleni.**

**…………………………………….**
**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**

**……………………………………..**
**SAHIHI MKUU WA SHULE.**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI BALANG'DALALU**

**KIAMBATANISHO "A"**

**FOMU YA KUKUBALI**

**MWANAFUNZI AJAZE FOMU HII**

Mimi …………………………………msichana/mvulana ninakubali kuingia kidato cha tano shule ya sekondari Balang'dalalu.

Tarehe………………… na nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii sheria za shule na nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kwenye kazi za nje, Mungu nisaidie.

Anuani yangu ya kudumu ni;

…………………………….

Sahihi ya mwanafunzi……………………..

**<u>MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII.</u>**

Mimi………………………………….. nakubali mtoto wangu………………………(jina) asome katika shule ya sekondari Balang'dalalu.
Naahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyooneshwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule hii.
Naahidi kuwa nitamsihi kutii sheria zote za shule na kuwa na bidii kwenye masomo na kwenye kazi za nje pia.
Anuani yangu ya kudumu ni;

……………………………

………………………….

…………………………

Sahihi ……………………………. Tarehe ………………………….

Wageni ninaowaidhinisha kuja kumuona mwanangu awapo shuleni muda maalumu uliopangwa na shule ni kila jumamosi na jumapili za mwisho wa miezi tu (wasizidi wawili)

| JINA | UHUSIANO |
|---|---|
| ………………………………….. | ……………………………………… |
| …………………………………. | …………………………………….... |